

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA



**MWONGOZO WA UOMBAJI NA UTOAJI WA LESENI KWENYE
VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO (SACCOS)**

Imeandaliwa na;
Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika,
S.L.P 201,
DODOMA.

Barua pepe: ushirika@ushirika.go.tz
Tovuti: www.ushirika.go.tz

Juni, 2020

VIFUPISHO

SACCOS Savings and Credit Co-operative Society

FICOS Financial Instituion Cooperative Society

YALIYOMO

VIFUPISHO.....	1
DIBAJI.....	4
SEHEMU YA KWANZA.....	6
UTANGULIZI.....	6
1.0 CHIMBUKO.....	6
1.1 DHANA YA UTOAJI WA LESENI.....	8
1.2 MADHUMUNI YA UTOAJI WA LESENI.....	8
SEHEMU YA PILI.....	9
MAOMBI YA LESENI.....	9
2.1 VIGezo VYA KUOMBA LESENI.....	9
2.1.1 Vigezo vya SACCOS kuomba Leseni - Daraja A.	9
2.1.2 Vigezo vya kupata Leseni - Daraja B.	10
2.2 HATUA ZA UOMBAJI WA LESENI.....	11
2.3 MAJUKUMU YA AFISA USHIRIKA - SEHEMU YA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA WA KIFEDHA ALIYEPOKEA MAOMBI YA LESENI.	11
2.4 TATHIMINI YA MAOMBI YA LESENI.....	12
2.5 UTOAJI WA LESENI.....	12
2.6 SACCOS KUKATALIWA KUPEWA LESENI.....	12
SACCOS KUKATA RUFEE.....	13
2.8 KUFUTWA KWA LESENI.....	13
SEHEMU YA TATU.....	14
3.0 BIDHAA NA HUDUMA ZINAZORUHUSIWA KUTOLEWA NA SACCOS.....	14
3.2 SACCOS ZENYE LESENI DARAJA B.....	14

3.3 BIDHAA NA HUDUMA AMBAZO HAZIRUHUSIWI KUTOLEWA NA SACCOS ZA
MADARAJA YOTE ISIPOKUWA KWA IDHINI YA MRAJIS 14

3.4 UTARATIBU WA SACCOS KUFUNGUA MATAWI 15

VIAMBATISHO 27

DIBAJI

Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) ni miongoni mwa aina ya Vyama vya Ushirika ambavyo vilianza kushamiri mwanzoni mwa miaka ya 1960. Vyama hivi vimekuwa vikisajiliwa na kusimamiwa na Mrajis wa vyama vya Ushirika chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ambayo imekuwa ikifanyiwa maboresho katika vipindi tofauti tofauti kutokana na mahitaji yanayoendana na wakati.

Pamoja na kuwepo kwa Sheria tajwa, usimamizi wa SACCOS umekuwa na changamoto mbalimbali ambazo zimedhoofisha maendeleo yake. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na uelewa mdogo wa wanachama juu ya usimamizi na ushiriki kwenye shughuli za chama, kutokuwepo kwa miongozo stahiki ya usimamizi, na baadhi ya wajumbe wa Bodi na watendaji kutokuwa na sifa na weledi wa kutosha katika usimamizi na uendeshaji wa shughuli za SACCOS. Aidha, baadhi ya SACCOS zimekuwa zikitoa huduma au bidhaa mbalimbali ikiwemo kufungua matawi au kufanya shughuli za uwakala na mikopo shirikishi bila kuzingatia uwezo wa mtaji na mifumo ya kusimamia na kutoa huduma hizo. Hali hii inaweza kusababisha fedha za wanachama kuwa kwenye hatari ya kupotea na kuathiri sekta ya fedha nchini.

Katika harakati za kuimarisha usimamizi wa SACCOS, Serikali imekuwa ikuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutunga Sera ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000 kwa lengo la kuimarisha sekta ya huduma ndogo za fedha na kufanya mapitio na maboresho ya Sera na Sheria ya Vyama Vya Ushirika. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania ilitunga Kanuni za taasisi za ushirika wa kifedha (FICOS) za mwaka 2005 kwa ajili ya kuzipatia leseni na kuzisimamia SACCOS zenye mtaji unaoanzia shilingi milioni mia nane (TZS 800,000,000) kwa lengo la kuimarisha usimamizi na kupunguza vihatarishi vya kifedha. Pamoja na jitihada hizo, hakuna SACCOS iliyowahi kuomba na kupatiwa leseni kutokana na kuwepo kwa mkanganyiko wa baadhi ya vipengele vilivyokuwemo katika kanuni hiyo hususan suala la mtaji na umiliki wa hisa.

Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iliandaa Sera ya taifa ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2017 baada ya mapitio ya Sera ya taifa ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2000. Lengo la Sera hiyo ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa utoaji wa huduma ndogo za fedha, uhamasishaji na uendelezaji wa huduma ndogo za

fedha na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Sera hii imeweka Mazingira wezeshi kwa wananchi kuendesha shughuli za kiuchumi na kijamii ambazo husaidia kuchangia ukuaji wa uchumi, kuongeza ajira na kupunguza umaskini nchini.

Sera ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2017 ilielekeza kutungwa kwa Sheria ya Usimamizi na Udhhibiti wa sekta ya huduma ndogo za fedha ikiwemo SACCOS ili kulinda watumiaji wa huduma hizo na kuondoa changamoto za kisheria zilizokuwepo katika kusimamia sekta hiyo. Kwa kuzingatia Sera hiyo, Serikali kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilitunga Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na.10 ya mwaka 2018. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania ilitunga Kanuni za usimamizi wa taasisi za huduma ndogo za fedha za mwaka 2019. Sheria na Kanuni hizo zilitangazwa na Waziri mwenye dhamana ya Fedha kuanza kutumika rasmi mnamo tarehe 01 Novemba, 2019.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria tajwa, Benki Kuu ya Tanzania imepewa mamlaka ya kukasimisha majukumu na mamlaka yake kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kusimamia shughuli na biashara ya huduma ndogo za fedha zinazolewa na SACCOS nchini. Kwa kuzingatia matakwa ya Sheria hiyo, Benki Kuu ya Tanzania ilikasimisha mamlaka na majukumu yake kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika mnamo tarehe 22, Novemba 2019 kupitia Gazeti la Serikali Na. 887.

Hivyo, Ili kutekeleza majukumu hayo, Mrajis wa Vyama vya Ushirika kwa mamlaka aliyonayo chini ya Sheria ya Vyama Vya Ushirika, Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha pamoja na kanuni zake, ameandaa mwongozo huu kwa ajili ya kuelekeza utaratibu, vigezo na masharti yatakayozingatiwa wakati wa kuomba na kutoa leseni kwenye SACCOS kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha pamoja na Kanuni zake.

Ni matarajio yangu kuwa kila SACCOS itazingatia utaratibu na maelekezo yaliyotolewa kwenye mwongozo huu kwa lengo la kufanikisha zoezi la uombaji na utoaji wa leseni kwenye SACCOS zote nchini.



Dkt. Benson O. Ndiege
MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 CHIMBUKO

Taasisi za Huduma Ndogo za fedha nchini zinajumuisha Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS). Wananchi wengi wamekuwa na imani na SACCOS na kuendelea kuzitumia kama njia muafaka ya kukidhi mahitaji yao ya kifedha na kijamii katika maeneo ya mjini na vijijini. Kundi kubwa la wananchi wanaojiunga na ‘SACCOS’ ni la wenye vipato vya kati na chini ambalo limeweka matarajio makubwa katika vyama hivi. Mbali na changamoto ya soko huria, ushindani mkubwa katika biashara ya fedha pamoja na mtikisiko wa uchumi uliozikabili taasisi nyingi za kifedha Duniani, bado ‘SACCOS’ zimeendelea kuwepo na kukidhi mahitaji ya wanachama wake. Hata hivyo, SACCOS zinatakiwa kuboresha uendeshaji na usimamizi wa shughuli zake ili ziweze kushindana na taasisi nyingine za kifedha katika kutoa huduma zilizo bora na kwa wakati kwa wanachama wake.

Pia, SACCOS nyingi nchini zinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo mitaji midogo, idadi ndogo ya wanachama, uwekezaji mdogo katika hisa, Akiba na mikopo, uandishi na utunzaji usioridhisha wa hesabu na kumbukumbu za Vyama, ukosefu wa baadhi ya viongozi na watendaji wenye weledi, ubunifu na uaminifu, ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, Sera, miongozo na Masharti ya Vyama. Pia SACCOS zimeshindwa kuweka matengo kwenye akaunti maalum, uwepo wa mikopo isiyorejeshwa kwa wakati, kutoainishwa kwa umri wa mikopo pamoja na kutotumia mifumo mizuri ya kutunza kumbukumbu ikiwamo TEHAMA.

Katika kukabiliana na changamoto hizi, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iliandaa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017 baada ya mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2000. Lengo la Sera hiyo ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa utoaji wa huduma ndogo za fedha, uhamasishaji na uendelezaji wa huduma ndogo za fedha pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Sera hii imeweka Mazingira wezeshi kwa wananchi kuendesha shughuli za kiuchumi na kijamii ambazo husaidia kuchangia ukuaji wa uchumi, kuongeza ajira na kupunguza umaskini nchini.

Sera hiyo ilielekeza kutungwa kwa Sheria ya Usimamizi na Udhhibiti wa sekta ya huduma ndogo za fedha ikiwemo SACCOS ili kulinda watumiaji wa huduma hizo na kuondoa changamoto za kisheria zilizokuwepo katika kusimamia sekta hiyo. Kwa kuzingatia Sera hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Fedha ilitunga Sheria ya huduma ndogo za Fedha ya mwaka 2018. Aidha, Benki kuu ya Tanzania ilitunga Kanuni za usimamizi wa taasisi za huduma ndogo za fedha za mwaka 2019.

Sheria na Kanuni hizo zilitangazwa na Waziri mwenye dhamana ya Fedha kuanza kutumika rasmi mnamo tarehe 01 Novemba, 2019. Kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria, Benki Kuu imepewa mamlaka ya kukasimisha majukumu na mamlaka yake kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kusimamia shughuli za SACCOS nchini. Kwa kuzingatia matakwa hayo ya Sheria, Benki kuu ilikasimisha mamlaka na majukumu yake kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika mnamo tarehe 22, Novemba 2019 kupitia Gazeti la Serikali Na. 887.

Hivyo, Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika imepewa nguvu na mamlaka ya kusimamia shughuli za SACCOS ikiwemo utoaji wa leseni kwa SACCOS kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za huduma ndogo za fedha.

Kutokana na umuhimu huo, na mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Sheria na Kanuni ya Vyama Vya Ushirika na Huduma Ndogo za Fedha, Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika imeandaa mwongozo utakaoweza walengwa wa mwongozo kutekeleza majukumu yao. Walengwa wa mwongozo huu ni pamoja na Warajis Wasaidizi, Maafisa Ushirika, SACCOS na wadau mbalimbali kujua vigezo, Masharti, taratibu nzima za uombaji, utoaji wa leseni na uendeshaji wa SACCOS zenyewe.

Matokeo ya utoaji wa leseni yataongeza ufanisi katika usimamizi wa SACCOS, utoaji huduma kwa wanachama na upatikaji wa takwimu za SACCOS. Hii itaongeza imani kwa wananchi katika kutumia huduma za SACCOS na kuchangia kipato cha nchi.

1.1 DHANA YA UTOAJI WA LESENI

Utoaji wa leseni kwa SACCOS ni utaratibu ambao umewekwa kwa ajili ya kuimarisha shughuli za usimamizi na uratibu wa SACCOS ambapo SACCOS inaomba na kupewa leseni kwa ajili ya kutoa huduma ndogo za fedha kwa kuzingatia matakwa ya Sheria na Kanuni za huduma ndogo za fedha. Leseni hiyo inaweza kuongeza wigo wa shughuli za SACCOS katika kutoa bidhaa/huduma za ziada kwa wanachama wake kwa kuzingatia mahitaji ya wanachama na matakwa ya Sheria. Aidha, leseni zitakazotolewa kwa SACCOS zitakuwa katika madaraja mawili (SACCOS zenye Leseni Daraja A na SACCOS zenye Leseni Daraja B) kutegemeana na uwezo wa chama kimtaji.

1.2 MADHUMUNI YA UTOAJI WA LESENI

Madhumuni ya utoaji wa Leseni kwa SACCOS ni pamoja na: -

- i. Kuboresha usimamizi na udhibiti wa shughuli za SACCOS,
- ii. Kuongeza wigo wa SACCOS kuendesha shughuli zake kwa kutoa huduma mbalimbali za kifedha,
- iii. SACCOS kujiendesha kwa weledi na kusimamiwa na viongozi na watendaji wenye sifa ambao watasaidia kubuni bidhaa na huduma mbalimbali kwa ajili ya kukidhi matakwa ya wanachama wake na
- iv. Kurahisisha upatikanaji wa taarifa.

SEHEMU YA PILI

MAOMBI YA LESENI

2.1 VIGEZO VYA KUOMBA LESENI

Chama chochote cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.06 ya mwaka 2013 kitatakiwa kuomba leseni ya utoaji wa huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na. 10 ya mwaka 2018 na Kanuni zake. Kwa mujibu wa Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (SACCOS) za mwaka 2019, SACCOS inaweza kuomba leseni daraja A au daraja B kutegemeana na vigezo vilivyoainishwa kwenye Sheria na Kanuni hizo. Ili SACCOS iweze kupewa leseni hiyo, lazima ikidhi vigezo vilivyoainishwa katika Kanuni ya 5(1) ya Kanuni za huduma ndogo za fedha kama ifuatavyo: -

2.1.1 Vigezo vya SACCOS kuomba Leseni - Daraja A.

Ili kupata Leseni daraja A, SACCOS itapaswa kuwa na sifa na nyaraka zifuatazo: -

- i. Mtaji tete (Core Capital) usiopungua shilingi milioni kumi.
- ii. Barua ya maombi kama ilivyoelekezwa katika Fomu Na.1 ya Jedwali la Kwanza la Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha za mwaka 2019
- iii. Majina na anwani kamili za wajumbe wa Bodi, Kamati ya usimamizi na maafisa waandamizi wa chama.
- iv. Wasifu binafsi wa wajumbe wa Bodi, Kamati ya usimamizi na Maafisa waandamizi wa chama.
- v. Nakala ya kitambulisho cha taifa, kitambulisho cha mpiga kura, hati ya kusafiria (passport) au kitambulisho chochote kitakachokubaliwa na Tume cha kila mjumbe wa bodi na maafisa waandamizi wa chama
- vi. Picha mbili (passport size) za kila mjumbe wa bodi na maafisa waandamizi wa chama.
- vii. Nakala iliyothibitishwa kisheria ya Masharti ya chama inayokidhi vigezo vya kupewa leseni.
- viii. Nakala ya hati ya usajili wa chama.
- ix. Nakala ya Sera ya mikopo
- x. Uthibitisho wa vifaa vya kutunzia fedha vyenye usalama na ulinzi wa kutosha na uwepo wa bima ya fedha hizo.

- xi. Nakala za taarifa ya ukaguzi wa hesabu kwa miaka miwili iliyopita.
- xii. Muhtasari wa Mkutano Mkuu uliyoidhinisha maombi ya leseni.
- xiii. Nakala ya uthibitisho wa ajira ya Mkaguzi wa Ndani au Mkataba wa mtoa huduma ya Mkaguzi wa Ndani.
- xiv. Uthibitisho wa uwepo wa mfumo wa TEHAMA ambao utaweza: -
 - o Kutoa taarifa za mwezi kuhusu Mapato na matumizi, Mizania, mikopo iliyocheleweshwa na umri wa mikopo.
 - o Kukidhi matakwa ya Kisheria ya utoaji wa taarifa ya kila mwezi.
 - o Kutoa utaratibu na maelezo kwa ajili ya miamala ya ziada inayohusu bidhaa na huduma mpya zitakazotolewa.
- xv. Nakala ya uthibitisho wa malipo ya shilingi 100,000/= kwa ajili ya maombi ya leseni. Ikumbukwe kuwa, Gharama hizo, hazitorejeshwa hata kama SACCOS itakosa Leseni.

2.1.2 Vigezo vya kupata Leseni - Daraja B.

Ili kupata Leseni daraja B, SACCOS itapaswa kuwa na sifa au nyaraka zote zilizoelzwa kwenye maombi ya leseni Daraja A pamoja na kuambatisha taarifa za mambo yafuatayo: -

- i. Mtaji tete (Core Capital) usiopungua shilingi milioni mia mbili.
- ii. Nakala za Sera ya mikopo, Uwekezaji, Rasilimali watu, Akiba, Ukwasi, Fedha, Mwongozo wa udhibiti wa ndani na taratibu zake
- iii. Nakala ya mpango mkakati wa miaka mitatu ikijumuisha dhima, muundo wa Utawala, bidhaa na huduma, mpango wa upanuzi wa matawi, mkakati wa ukuaji, makisio ya Mapato na Matumizi, Mizania, mtiririko wa fedha na vigezo vilivyotumika kufanya makisio hayo.
- iv. Uthibitisho kwamba, kuna usalama wa kutosha wa mali za chama
- v. Nakala ya uthibitisho wa malipo ya shilingi 300,000/= kwa ajili ya maombi ya leseni. Ikumbukwe kuwa, Gharama hizo, hazitorejeshwa hata kama SACCOS itakosa Leseni.

2.2 HATUA ZA UOMBAJI WA LESENI

SACCOS itapaswa kuwasilisha maombi yake katika ofisi za ushirika zilizo karibu au kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika (<https://www.ushirika.go.tz>, sehemu ya maombi ya leseni - *License Application*).

Afisa Ushirika atakayepokea maombi hayo, atapaswa kupitia nyaraka na kuthibitisha kwamba: -

- i. Maombi yamewasilishwa kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa kwenye maombi ya leseni husika na fomu iliyopo kwenye jedwali la kwanza la Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha za SACCOS (Kiambatisho A) imejazwa kwa ukamilifu;
- ii. Maombi yamesainiwa na Mwenyekiti wa Chama;
- iii. SACCOS imelipa ada ya maombi ya leseni kiasi cha Sh. 100,000 kwa leseni Daraja A au Sh. 300,000 kwa leseni Daraja B.

2.3 MAJUKUMU YA AFISA USHIRIKA - SEHEMU YA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA WA KIFEDHA ALIYEPOKEA MAOMBI YA LESENI.

Afisa ushirika aliyepokea maombi ya leseni, atapaswa kufanya uchambuzi wa maombi hayo kwa kuzingatia Mahitaji au Masharti yaliyoelezwa sehemu ya 1.5.1 na 1.5.2 ya mwongozo huu ili kubaini na kuthibitisha uhalali wa nyaraka husika. Afisa Ushirika atafanya uchambuzi wa taarifa zilizowasilishwa na kutoa taarifa yake kwa Mrajis.

- i. Pale Afisa Ushirika atakapobaini maombi yamekamilika, atamshauri Mrajis kukubali kupokea maombi na kwamba ndani ya siku 60 Mrajis ataamua ikiwa leseni inapaswa kutolewa au la.

- ii. Endapo Afisa Ushirika atabaini kwamba, nyaraka na taarifa zilizowasilishwa hazijakamilika na hazijakidhi vigezo, atamshauri Mrajis kwamba, mwombaji apewe muda wa kufanya maboresho kwa nyaraka zenye mapungufu au zilizokosekana ili kuweza kukidhi sifa na vigezo vya kupatiwa leseni. **(Kiambatisho B - barua ya maelekezo ya mapungufu na maboresho yanayohitajika).**

2.4 TATHIMINI YA MAOMBI YA LESENI

Kabla ya utoaji wa Leseni, Mrajis anaweza kufanya ukaguzi chamani ili kujiridhisha juu ya uhalali wa nyaraka na taarifa zilizowasilishwa na chama husika. Maeneo yanayoweza kufanyiwa ukaguzi ni pamoja na Jengo la Ofisi, vifaa vya mawasiliano, uhasibu na mifumo ya udhibiti wa ndani.

2.5 UTOAJI WA LESENI

Mrajis atatoa leseni kwa SACCOS ambazo zitakuwa zimekidhi matakwa na vigezo vilivyoainishwa katika mwongozo kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za huduma ndogo za fedha. Endapo SACCOS itakuwa imekidhi vigezo hivyo, Mrajis ataipatia leseni ndani ya siku 60 kwa kutumia **kiambatisho Na. C.**

2.6 SACCOS KUKATALIWA KUPEWA LESENI

- i. Pale Mrajis atakapona SACCOS haijakidhi sifa na vigezo vya kupewa leseni, atatakiwa ndani ya siku saba (7) baada ya kufanya maamuzi kuijulisha SACCOS hiyo sababu za kutopewa leseni. **(Kiambatisho Na. D)**
- ii. SACCOS ambayo maombi yake yamekataliwa inaweza kutuma maombi mapya kwa kurekebisha mapungufu yaliyosababisha kukataliwa kupewa leseni na maombi hayo yatachukuliwa kama maombi mapya ya Leseni.

2.7 SACCOS KUKATA RUFAA

SACCOS ambayo haijaridhishwa na uamuzi wa Mrajis wa kukataa kuipatia leseni inaweza kukata rufaa kwa Benki Kuu (BOT) ndani ya siku 21 kutoka tarehe ya kupokea notisi ikieleza mambo yafuatayo: -

- Aina ya pingamizi
- Misingi ya Pingamizi
- Mambo mengine kadri chama kitakavyoona inafaa.

2.8 KUFUTWA KWA LESENI

SACCOS inaweza kufutiwa Leseni iwapo itashindwa kukidhi vigezo vilivyowekwa kwenye Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha. Zifuatazo ni sababu zinazoweza kusababisha Mrajis kufuta Leseni:

- a) Kuacha kutoa huduma ndogo za fedha
- b) Kukiuka taratibu na masharti yaliyoainishwa kwenye leseni
- c) SACCOS inafungwa, inafilisiwa au inavunjwa vinginevyo
- d) Imefutwa chini ya Sheria husika.
- e) Imekiuka matakwa ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha

Ndani ya siku kumi na nne (14) za kufuta leseni, Mrajis atapaswa kutangaza jina la chama kilichofutwa kwenye gazeti la serikali na magazeti ya habari ya kawaida yenye uwezo wa kuwafikia watu wengi nchini.

SEHEMU YA TATU

3.0 BIDHAA NA HUDUMA ZINAZORUHUSIWA KUTOLEWA NA SACCOS

3.1 SACCOS ZENYE LESENI DARAJA A zinaruhusiwa kutoa bidhaa na huduma zifuatazo;

- i. Hisa za lazima za Uanachama
- ii. Hisa za hiari
- iii. Akiba
- iv. Mikopo kwa wanachama
- v. Uwekezaji na;
- vi. Huduma nyingine kadri zitakavyoamuliwa na Mrajis.

3.2 SACCOS ZENYE LESENI DARAJA B

SACCOS zenye leseni Daraja B zitaruhusiwa kutoa huduma na bidhaa zifuatazo;

- i. Bidhaa na huduma zote zinazotolewa na SACCOS zenye leseni Daraja A
- ii. Kutoa Mikopo shirikishi.
- iii. Kupokea Amana za wanachama za muda maalum
- iv. Kutoa huduma za uwakala wa bima ndogo
- v. Kuwekeza kwenye soko la mitaji (Equity Investment)
- vi. Kuwa wakala wa benki kwa idhini ya Mrajis
- vii. Kutoa mikopo ya karadha ndogo (Microleasing)
- viii. Kutoa kadi za kutolea fedha (Debit Card)
- ix. Bidhaa na huduma nyingine kama itakavyoelekezwa na Mrajis.

3.3 BIDHAA NA HUDUMA AMBAZO HAZIRUHUSIWI KUTOLEWA NA SACCOS ZA MADARAJA YOTE ISIPOKUWA KWA IDHINI YA MRAJIS

- i. Uendeshaji wa akaunti ya akiba kwa wanachama wake;
- ii. Kupokea amana kutoka kwa wasio wanachama
- iii. Biashara ya kubadilisha fedha za kigeni;
- iv. Uendeshaji wa biashara za nje ya nchi;
- v. Shughuli za udhamini;
- vi. Maagizo ya malipo na uhamishaji wa fedha;
- vii. Kadi za kununulia bidhaa kwa mkopo (Credit Card);

- viii. Shughuli yoyote tofauti na utoaji wa bidhaa na huduma za kifedha kwa wanachama wake; na
- ix. Shughuli nyingine kama itakavyoelekezwa na Mrajis

3.4 UTARATIBU WA SACCOS KUFUNGUA MATAWI

SACCOS yenye Leseni daraja B inayokusudia kufungua tawi ili kupanua uendeshaji wa shughuli zake, itapaswa kuomba idhini ya maandishi kwa Mrajis. Maombi yatakayowasilishwa yataambatishwa na mambo yafuatayo;

- i. Eneo linalopendekezwa kwa ajili ya kufungua tawi;
- ii. Lengo na madhumuni ya kufungua tawi jipya;
- iii. Bajeti yenye mchanganuo na chanzo cha fedha za uanzishwaji wa tawi;
- iv. Makisio (projected) ya Mizania na Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa muda wa miaka miwili baada ya tawi kuanza;
- v. Mapendekezo ya muundo wa tawi, majina na wasifu binafsi wa waajiriwa muhimu katika tawi; na
- vi. Taarifa nyingine kama Mrajis atakavyoelekeza.

Mrajis hataruhusu SACCOS yenye leseni daraja B kufungua tawi mpaka atakopojiridhisha kuwa sehemu husika inafaa kufunguliwa tawi. Aidha, kabla ya kuruhusu SACCOS kufungua tawi mambo yafuatayo yatazingatiwa ikiwa ni pamoja na;

- i. Uwezo wa kujiendesha kwa tawi linalopendekezwa
- ii. Uwezo wa kifedha wa SACCOS kuendesha tawi linalopendekezwa.
- iii. Endapo SACCOS inakidhi vigezo vya chini vya mtaji
- iv. Ustadi na uwezo wa watendaji wa tawi linalopendekezwa
- v. Endapo tawi linalopendekezwa linakidhi vigezo kwa kiwango cha chini cha mahitaji ya usalama
- vi. Masuala mengine yoyote kama itakavyobainishwa na Mrajis

3.5 KUBADILI SEHEMU YA BIASHARA

SACCOS ambayo inakusudia kubadili sehemu ya biashara yake itapaswa kuomba idhini kwa maandishi kutoka kwa Mrajis. Maombi hayo yataambatishwa na taarifa zifuatazo; -

- i. Sababu za kubadili sehemu ya biashara
- ii. Mpango wa kulipa au kuhamisha madai, mali na madeni.
- iii. Ukamilishaji wa maandalizi ya sehemu mpya ya biashara
- iv. Taarifa nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na Mrajis.

3.6 KUFANYA SHUGHULI ZA MLANGO WA HUDUMA (OUTLETS SERVICES)

SACCOS hairuhusiwi kufungua au kuendesha mlango wa huduma bila idhini ya maandishi ya Mrajis iliyotolewa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha zinazosimamia SACCOS. Ombi la idhini litakalowasilishwa na SACCOS kwa ajili ya kufanya shughuli za mlango wa huduma zitaambatisha taarifa zifuatazo: -

- i. Sifa za kiusalama na nafasi iliyopo kwa ajili ya SACCOS kutoa bidhaa na huduma
- ii. Taarifa nyingine yoyote kama Mrajis atakavyoelekeza.

HITIMISHO

Mwongozo huu ni muhimu katika uombaji na utoaji wa leseni za SACCOS nchini kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa SACCOS kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha. Aidha, mwongozo huu unapaswa kuzingatiwa na wadau wote kwa lengo la kuwezesha ofisi ya Mrajis, Bodi, Watendaji na Wadau mbalimbali ili kuhakisha SACCOS zinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria. Kushindwa kutekeleza maelekezo na masharti yaliyoainishwa kwenye mwongozo huu ni kwenda kinyume na matakwa ya Sheria na SACCOS husika inaweza kuwajibishwa kwa kwenda kinyume na maelekezo yaliyotolewa kwenye mwongozo huu.

Aidha, SACCOS zote zinapaswa kuhakikisha zinakamalisha maandalizi ya utekelezaji wa Sheria ikiwa ni pamoja na kuhakikisha zinaomba na kupatiwa leseni kwa mujibu wa Sheria. Kutungwa kwa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha pamoja na Kanuni zake, kunategemea kuongeza hamasa kwa watoa huduma na kuongeza ubunifu wa bidhaa na huduma zinazotolewa kwa wanachama ili ziweze kukidhi mahitaji yao ya kiuchumi na kijamii. Ofisi ya Mrajis itaendelea kuhakikisha kuwa taratibu za usimamizi na uendeshaji wa shughuli za SACCOS zinafuatwa ili kupata matokeo yenye tija kwa wanachama na jamii kwa ujumla nchini.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA**

FOMU Na. A

(Chini ya Kanuni ya 14(2)(b))

FOMU YA MAOMBI YA LESENI

1. Jina la SACCOS.....
 Namba ya Usajili.....
 Tarehe ya usajili.....
2. Mahali ilipo Ofisi iliyosajiliwa:
3. Anwani ya mahali ilipo Ofisi ya Makao Makuu: L.R. Na.....
 Mtaa:
 Jengo:
4. Anwani ya posta.....Geresho la Posta.....
 Namba ya Simu.....
 Barua Pepe.....
5. Majina ya maeneo ya biashara katika Tanzania na miaka ambayo kila eneo
 lilianzishwa na kufanya biashara.....

<i>Na.</i>	<i>Jina la Tawi</i>	<i>Mwaka wa Kuanzishwa</i>	<i>Idadi ya miaka ya kufanya kazi</i>
1.			
2.			
3.			
4.			

5.			
----	--	--	--

NB: Ambatisha pamoja na maombi haya orodha ya maeneo mengine ya biashara. Ainisha majina ya maeneo ya biashara aina kama ni ya setelaiti, Kitengo Tembezi, ATM au Kituo cha Mauzo.

6. Majina ya zamani, kama yapo, ambayo yalitumiwa na SACCOS:

Na.	Jina	Mwaka wa Kutumika	
		Kutoka	Hadi
1.			
2.			
3.			
4.			

7. Maelezo ya mtaji:

(a). Idadi na thamani ya hisa zilizolipiwa.....

(b). Mtaji Tete.....

8. Taarifa za Maafisa:

(a). Wajumbe wa Bodi:

Na.	Majina	Tarehe ya Kuzaliwa	Elimu/Weledi		Tarehe ya Kuchaguliwa	Nafasi nyingine anazoshikilia
			Kiwango	Mwaka wa kuipata		
1.						
2.						
3.						
4.						

5.						
----	--	--	--	--	--	--

(b). Watendaji Waandamizi:

Na.	Majina	Cheo	Tarehe ya Kuzaliwa	Elimu/Weledi		Tarehe ya Kuajiriwa	Ajira ya Kabla
				Kiwango	Mwaka wa kuipata		
1.							
2.							
3.							
4.							
5.							
6.							
7.							

9. Majina na Anwani za Benki:

Na.	Jina la Benki	Anwani	Namba ya Simu	Barua Pepe
1.				
2.				
3.				
4.				
5.				

10. SACCOS ilishawahi kuwekwa chini ya uangalizi au kufanya maafikiano au mapatano na wadai wake au vinginevyo kushindwa kulipa wadai wake?..... ikiwa ndiyo, toa maelezo yake

MFANO WA BARUA YA MAOMBI YA LESENI

Bodi ya SACCOS
S.L.P XXXX
DODOMA
TANZANIA

Tarehe.....

Kumb. Na.....

Mrajis Tume ya Maendeleo ya Ushirika,
S.L.P 201,
DODOMA,
TANZANIA

**Yah: MAOMBI YA LESENI DARAJA..... KWA AJILI YA KUENDESHA SHUGHULI
ZA CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO**

Rejea kichwa cha habari hapo juu

2. Chama cha ushirika wa akiba na mikopo kwa kuzingatia Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 pamoja na Kanuni zinasosimamia SACCOS kupitia Sheria hiyo, tunaleta maombi husika ili chama chetu kilichosajiliwa kwa jina la kiweze kupatiwa leseni. Chama hiki kitaendesha shughuli zake katika Mkoa wa Wilaya ya kata ya.....

3. Ili kuweza kujiridhisha kama chama chetu kimekidhi sifa na vigezo vya kupatiwa leseni nimeambatisha vielelezo muhimu kama ilivyoelekezwa kwa rejea yako.

4. Tukiwa kama Bodi ya chama, tumepitia na kujiridhisha pasipo shaka kwamba vielelezo vilivyowasilishwa ni sahihi kwa ufahamu wetu. Aidha, tunaiomba ofisi yako iweze pia kujiridhisha juu ya uwepo wetu pamoja na vielelezo tulivyowasilisha kwa namna bora vile ambavyo itakavyoonekana inafaa.

5. Pamoja na barua hii nimeambatisha, vielelelzo husika ikiwa ni pamoja na hati ya uthibisho wa malipo ya maombi ya leseni ya Tsh.....

“Pamoja na Salamu za Ushirika”

.....

Jina la Mwenyekiti wa Chama.

KIAMBATISHO B

BARUA YA MAELEKEZO KUHUSU MAPUNGUFU NA MABORESHO YANAYOTAKIWA
KUFANYWA NA SACCOS ILI IWEZE KUPATIWA LESENI.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika
S.L.P 201,
DODOMA

Kumb Na.....

Tarehe

Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,
Bodi ya XXXX SACCOS LTD,
S.L.P XXXXX,
DODOMA.
TANZANIA.

**Yah: MAOMBI YA LESENI DARAJA KWA AJILI YA KUENDESHA
SHUGHULI ZA CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO**

Rejea barua yenu ya tarehe.... yenye Kumbukumbu Na.....kama kichwa
cha habari hapo juu kinavyoeleza kuhusu maombi ya kupatiwa leseni ya
SACCOS daraja.....

Ofisi ya Mrajis ilipokea na kuchambua maombi husika kama mlivyowasilisha
ili muweze kupatiwa Leseni ya kuendesha biashara ya huduma ndogo za
fedha. Baada ya kufanyika kwa upembuzi wa awali, SACCOS yenu imebainika
kuwa na mapungufu yafuatayo;

- i.
- ii.
- iii.

Hivyo ili muweze kupatiwa leseni husika, mnaelekezwa kuhakikisha
mnawasilisha nyaraka na kutoa ufafanuzi kwenye maeneo yaliyoainishwa
kama ifuatavyo;

- (a)
- (b)
- (c)

Nyaraka na ufafanuzi husika unapaswa kuwasilishwa ndani ya kipindi cha siku 30 tangu tarehe ya barua hii. Kushindwa kuzingatia muda na tarehe ya kuwasilisha nyaraka na ufafanuzi huo, kutasababisha maombi yenu yasitishwe na kutoendelea kufanyiwa kazi na ofisi ya Mrajis kutokana na kutowasilishwa kwa nyaraka hizo.

Nawatakia kazi njema.

“Pamoja na Salamu za Ushirika”

Benson O. Ndiege

MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA TANZANIA BARA

LESENI NA. MSP3 - LESENI YA KUFANYA BIASHARA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Imetolewa chini ya kifungu Na. 20 cha Sheria ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2018

DARAJA.....

Leseni hii imetolewa kwa SACCOS
Namba ya Usajili.....ya.....(anwani) na kuidhinisha SACCOS hii kutoa huduma ndogo za fedha Tanzania Bara katika daraja la tatu ikiwa na Leseni daraja

Leseni hii imetolewa kwa kuzingatia Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 na maelekezo yaliyopo kwenye barua yetu ya tarehe..... yenye Kumbukumbu Na..... ya tarehe

Imetolewa leo tarehe MweziMwaka.....

SAHIHI

Dar es Salaam,
....., 2019

BENSON OTIENO NDIEGE
MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA

KIAMBATISHO D

BARUA YA KUIJULISHA SACCOS SABABU ZA KUKATALIWA KUPEWA LESENI.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika
S.L.P 201,
DODOMA

Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,
Bodi ya XXXX SACCOS LTD,
S.L.P XXXXX,
DODOMA.
TANZANIA

**Yah: MAOMBI YA LESENI DARAJA..... KWA AJILI YA KUENDESHA SHUGHULI
ZA CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO LTD**

Rejea barua yako ya tarehe..... yenye Kumbukumbu Na.....kama kichwa cha habari hapo juu kinavyoeleza kuhusu maombi ya kupatiwa leseni ya SACCOS daraja.....

Ofisi ya Mrajis inasikitika kuwajulisha kuwa ombi lenu la kupatiwa leseni kwa ajili ya kuendesha bishara ya huduma ndogo za fedha limekataliwa. Aidha, sababu zilizopelekea SACCOS yenu ishindwe kupewa leseni ni pamoja na: -

- i.
- ii.
- iii.....
- iv.
- v. Nyingine (kama zipo)

Nawatakia kazi njema.

“Pamoja na Salamu za Ushirika”

Benson O. Ndiege

MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA